BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Sita – Tarehe 04 Disemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA.

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI) kwa mwaka 2023/2024.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI) kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

83. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Udhibiti na uhifadhi wa mazingira ni jambo la msingi kwa mustakabali wa maisha yetu na visiwa vyetu.

Ni upi mkakati wa Serikali juu ya udhibiti wa mazingira hasa tukizingatia kuwa binaadamu amekuwa kikwazo kikubwa katika uhifadhi wa mazingira.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

104. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Baadhi ya wafanyakazi wa taasisi zisizo za kiserikali hawapatiwi mikataba, vifaa kwa ajili ya usalama na afya kazini na kunyimwa haki zao nyengine.

Je, utambuzi wa Wizara yako uko vipi juu ya matatizo hayo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

130. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wawanake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Lengo la viongozi wetu ni kuona vijana wao wanapata ukakamavu na mafunzo stadi mbali mbali kupitia kambi zake za J.K.U. na J.K.T. kwa muda wa miezi 6 hadi mwaka 1 hapo awali.

Ni sasabu zipi zilizofanya vijana hawa kuwepo kambini kwa muda wa miaka 2 sasa.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

7. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

(a) Kwa ufupi ni yepi matumizi haramu ya fedha ya Kitanzania.

(b) Ni hatua gani za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa kwa mwananchi anayeidhalilisha na kuitoa thamani fedha halali ya Kitanzania.

127. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na uhaba mkubwa wa ofisi kwa taasisi za Serikali zilizopo Pemba, jambo ambalo limezifanya takribani taasisi zote na Wizara kubanana sehemu moja katika eneo la Gombani-Chake. Jambo hili linaathiri utendaji wa taasisi hizi katika kutoa huduma bora kwa wananchi na kuleta malalamiko.

(a) Kwa kuwa Serikali inalitambua tatizo hili la uhaba wa ofisi, je, imefanya tathmini na kujiridhisha ni Wizara na taasisi ngapi zilizopo pamoja katika eneo hili la Gombani-Chake.

(b) Je, Serikali inachukuwa hatua zipi ili kutatua tatizo hili na kuboresha huduma kwa wananchi.

(c) Kwa kuwa sehemu nyingi Serikali hupanga miji ya kiserikali, Je, kwa Pemba ni eneo gani lililopangwa kwa shughuli za ujenzi wa ofisi za Serikali na hatua za ujenzi huo zipo vipi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

48. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Tathmini iko vipi juu ya mabadiliko ya miundombinu ya ujenzi mpya wa skuli za ghorofa yanayoendelea kuimarika nchini.

(b) Je, kwa kiasi gani ujenzi wa skuli hizo za ghorofa unapelekea ongezeko la ufaulu wa wanafunzi.

51. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tathmini ya tatizo la utoro mashuleni kwa sasa linachukua sura na taswira gani.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

107. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kila mwaka kumekuwa na matokeo mengi ya kuzama na kupotea kwa vyombo vya baharini vinavyofanya safari baina ya Tanga, Kenya na Pemba. Changamoto hii imepelekea upotevu wa maisha kwa mabaharia na mali nyingi za wafanyabiashara wanaofanya biashara zao Pemba.

(a) Je, tathimini inaonesha ni vyombo vingapi vimepotea ama kuzama katika safari zake tokea mwaka 2020 na watu wangapi waliokolewa na vyombo vya uokozi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kupunguza vifo vinavyotokana na ajali hizo za kuzama vyombo vya baharini.

112. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasilino na Uchukuzi.

Nchi nyingi duniani zimeanza mkakati wa kupunguza matumizi ya vyombo vya moto vinavyotumia mafuta na kuwekeza katika vyombo vya moto vinavyotumia umeme maarufu kama magari ya umeme (e-mobile).

(a) Je, Serikali imefanya tafiti kuhusu matumizi ya (e-mobile) Zanzibar.

(b) Ni ipi tathmini ya uingizaji wa vyombo vya moto vinavyotumia umeme Zanzibar.

(c) Je, ni mkakati upi wa Serikali katika kushawishi matumizi ya (e-mobile) hapa Zanzibar.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

38. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Tathmini ya mauzo ya ving'amuzi vya ZMUX kwa sasa iko vipi.

39. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Hapo zamani kulikuwa na gazeti la vichekesho likikemea na kuwaadhibu wale wote wanaoikosea na kuidhihaki au kuifuja lugha ya Kiswahili maarufu kama Kifimbocheza.

    Kwa sasa ni nani anaebeba mamlaka ya uhusika wa Kifimbocheza katika tasnia mbali mbali hususan katika vyombo vya habari hapa nchini.

**Wizara ya Afya:**

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Tafiti zinaonesha kuongezeka kwa tatizo la watoto wenye udumavu.

    (a) Ni athari gani za kiafya na kijamii zinazowapata watoto wenye udumavu.

    (b) Ni umri wa miaka mingapi akifikia mtoto tatizo hili halitawezekana tena.

    (c) Nini kifanyike kuondokana na tatizo hili la watoto wenye udumavu tangu ujauzito wa mama kutunga mpaka mtoto kuzaliwa.

25. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    (a) Kwa sasa tuna madaktari wangapi wa ganzi (anesthesia) wanaohusika na maandalizi ya huduma za mgonjwa kufanyiwa upasuaji katika hospitali zetu.

    (b) Ni upi umuhimu wao kwa ujumla.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

29. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ni vipi Wizara yako inafanya vipimo na kujiridhisha juu ya uwepo wa viwango bora vya mafuta katika sheli zetu.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

53. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ni katika mazingira gani, maeneo yepi na kwa nyakati zipi mtoto hatakiwi kuonekana akizurura au akiranda nje ya nyumbani kwao, kwa mujibu wa sheria na kanuni za kumlinda mtoto.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

18. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Kwa kuzingatia tathmini iliyopo, je ni wanyama gani wametoweka au wanatoweka kutokana na mazingira ya kuhusishwa na vitendo vya imani za kishirikina.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali juu ya ukatili kama huu unaowaingiza wanyama katika adhabu wasiyostahiki kuwa nayo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

63. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zanzibar ina historia ya kupigana vita vifupi zaidi duniani.

(a) Kwa kiasi gani historia hii inaenziwa kama ni sehemu ya kivutio cha utalii.

(b) Ni mara ngapi na matokeo gani yamepatikana kutokana na kufanyika kwa uzamiaji (underwater archeology) katika eneo lililotumika kama ni uwanja wa vita hivi.

64. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kiasi gani malalamiko ya watoa huduma katika mahoteli mbali mbali ya kitalii (suppliers) hususani katika suala zima la mikataba limefanyiwa kazi.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Taarifa ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) kwa mwaka 2023/2024.

Taarifa ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI) kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**04 Disemba, 2024.** **KATIBU WA BARAZA.**